OFISI YA RAIS TAMISEMI
HALMASHAURI YA MJI KONDOA

Julai— Septemba 2022

# Wamshukuru Mhe. Rais kuwajengea kituo cha Afya Serya



Mhe. Samia Suluhu Hassan
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

SERA YA UHARIRI

Madhumuni ya Jarida hili ni kuhabarisha na kuelimisha wananchi juu ya shughuli mbalimbali zinazofanywa na Halmashauri ya Mji Kondoa. Aidha Sera, Mipango na utekelezaji wa miradi ya maendeleo inafafanuliwa kupitia jarida hili. Isipokuwa pale inapokatazwa habari za Jarida la Halmashauri ya Mji Kondoa zinaweza kunukuliwa ili mradi Mhariri ajulishwe kwa maandishi.

**Bodi ya Uhariri**

Paul Sweya

Sekela Mwasubila

Saumu Sakala

**Mawasiliano**

S.L.P 711 Kondoa

Simu: +255 712264912

Nukushi: +255262360313

**Mitandao ya Kijamii**

www: kondoatc.go.tz

Kondoa TC

kondoatc

Barua Pepe
td@kondoatc.go.tz

# NENO KUTOKA KWA MKURUGENZI



Paul Mamba Sweya

**Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Kondoa**

Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutufikisha hadi siku ya leo na kumaliza salama utekelezaji wa kazi zilizopangwa katika kipindi cha robo ya kwanza Julai—Septemba 2022.

Pili natoa shukrani za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Hassan kwa kutupatia fedha shilingi milioni 180 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 9 ya wanafunzi wa kidato cha kwanza 2023, shilingi milioni 150 kwa ajili ya ukarabati wa Shule ya Wasichana Kondoa na shilingi milioni 100 kwa ajili ya ukarabati wa Shule ya Msingi Kolowasi.

Vilevile katika kipindi cha robo ya kwanza Julai hadi Septemba 2022 Halmashauri ya Mji imepokea fedha kiasi cha Tshs. 910,329,558.46 kutoka katika vyanzo vya mapato mbalimbali ambapo kiasi cha Tshs. 73,145,000 mapato ya ndani ya Halmashauri, Shs. 485,628,262.46 kutoka Serikali kuu, Shs 351,556,296 toka kwa wahisani. Aidha Shs. 430,000,000 zimepokelewa nje ya bajeti.

Hadi kufikia mwezi Septemba 2022 Halmashauri ya Mji imetumia Shs. 422,849,558.46 katika utekelezaji wa shughuli za miradi ya Maendeleo kwa mchanganuo ufuatao

1. Shs. 11,000,000 mapato ya ndani zimepelekwa kwenye vikundi vya wanawake, watoto na watu wenye ulemavu.
2. Shs. 305,628,262.46 zimepelekwa kwenye maeneo husika ikiwemo mitihani na uboreshaji wa mazingira ya kujifunza na kufundisha.
3. Shs. 101,556,296 zimepelekwa katika shughuli za kuwezesha kaya maskini na shughuli.

Mwisho niwasihi wananchi wote wa Halmashauri ya Mji waliopokea fedha za utekelezaji wa miradi kuitekeleza kwa pamoja kwa kuzingatia kanuni, sheria na taratibu za matumizi ya fedha za miradi ikiwa ni pamoja na kutekeleza kwa kiwango cha hali ya juu kwa manufaa ya wanachi na watoto wetu.

**ASANTENI SANA!**

# BARAZA LA WAHESHIMIWA MADIWANI



Mhe. Mohamed Kiberenge
**Mwenyekiti wa Halmashauri**




Mhe. Ally Makoa
**Mbunge Kondoa Mjini**



**Mhe. Besela Maunga**
**M/Mwenyekiti wa Halmashauri**



Mhe. Zainabu Haroub
**Diwani kata ya Chemchem**



Mhe. Abushehe Mbuva
**Diwani Kata ya Kingale**



Mhe. Japhari Ganga
**Diwani Kata ya Suruke**



Mhe. Fatuma Issa
**Diwani V/M Kondoa Mjini**



Mhe. Ramla Abeid
**Diwani Kata ya Bolisa**



Mhe. Rachel Sombida
**Diwani V/M Kondoa Mjini**



Mhe.  Issa Kambi
**Diwani Kata ya Kilimani**



Mhe. Kulwa Pazi
**Diwani Kata ya Serya**



Mhe. Idd Ng'ungu
**Diwani Kata ya Kolo**



# Wamshukuru Mhe. Rais kuwajengea kituo cha Afya Serya

Wananchi wa kata ya Serya Halmashauri ya Mji Kondoa wamemshukuru Rais Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuwajengea kituo cha Afya kutokana na fedha za tozo za miamala ya simu ambapo kwasasa wanapata huduma katika kituo hicho.

Shukrani hizo wamezitoa wakati wa mahojiano yao na Afisa Habari alipotembelea katika kituo hicho kuona huduma zinazotolewa katika kituo hicho hivi karibuni.

"Kabla ya kujengwa kwa kituo hiki wakinamama wajawazito walikuwa wakipata changamoto kubwa wakati wa kujifungua hasa wakati wa masika mto Bubu ukijaa hawezi kuvuka kwenda kupata huduma Kondoa Mjini na wengine wamepoteza maisha kwa kweli hali ilikuwa mbaya,"amesema Anna Uruwa Mtendaji wa Mtaa wa Mongoroma kilipojengwa kituo hicho.

Ameongeza kwa kusema kuwa baada ya kujengewa kituo hicho wajawazito kwasasa hawapati shida kama awali kwani wanapata huduma zote katika kituo hicho hali ambayo pia imewasaidia kufanya shughuli zingine za kujiongezea kipato kwa kuwa huduma imesogezwa kwa karibu.

Kwa upande wake Bwana amesema pamoja na kupatikana kwa kituo hicho wanaomba kujengewa wodi ya wanaume na wanawake ili inapotokea mgonjwa anatakiwa kulazwa alazwe katika kituo hicho ikiwa ni pamoja na kuletewa wataalam wa afya wa kutosha.

Akizungumza awali Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji Kondoa Dkt. Sisty Mosha amesema huduma zitakazotolewa katika kituo hicho ni huduma ya mama na mtoto, huduma za macho, huduma za upasuaji mdogo, kliniki za mama na mtoto, wagonjwa wa nje na huduma meno.

Kituo cha Afya Serya kimejengwa kwa gharama ya shilingi milioni 500 fedha zilizoletwa kutoka serikali kuu na zimetokana na tozo za miamala ya simu ambapo majengo yaliyokamilika mpaka sasa ni jengo la wagonjwa wa nje, jengo la mama na mtoto, maabara, jengo la kufulia na kichomea taka na huduma zimeanza katika kituo hicho.



# Viongozi wa Shule Watakiwa kusimamia taratibu kuboresha

Wakuu wa shule, walimu wakuu na maafisa elimu kata wametakiwa kusimamia kanuni,sheria ns taratibu za elimu katika kusimamia taaluma ili kuinua taaluma na kuongeza kiwango cha ufaulu.

Kauli hiyo imetolewa na Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Kondoa Dkt. Khamis Mkanachi wakati wa hafla ya uzinduzi wa kitabu cha Mkakati wa kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji ngazi ya elimu msingi na kitabu cha Changamoto katika uboreshaji elimu msingi na Sekondari uliofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya Mji Kondoa hivi karibuni.

"Hakuna kusema watoto wa Kondoa hawapendi shule mnaamishia lawama kwa watoto lakini ukweli ni kwamba akifeli mtoto wote mmefeli hadi sisi viongozi wa Wilaya, ila nawaambieni mkiamua kwa dhati mnaweza ila ninachoona walimu wanadeka, wanafunzi nao wanadeka hadi wanafunzi wanadeka,"amesema Dkt. Mkanachi

Aidha amewaambia kuwa ufaulu wa mwanafunzi kwa asilimia kubwa unatokana na maamuzinya mwalimu kuanzia wa somo husika na wao pia wasipoamua mwanafunzi kufaulu hafaulu hivyo amewataka wote kukaa vikao katika shule zao na kusemana kwa ambao wanafanya vibaya ili wajirekebishe ikiwa ji pamoja na kuacha kuingiza siasa kwenye masuala ya taaluma.

Ameongeza kuwa wao kama wadaunwa elimu waguswe na matokeo mabaya ya wanafunzi tofauti na sasa baadhi yao hawaguswi hivyo amewaambia wao kama viongozi, wadau wa elimu na walimu dhana ya ufaulu ya wote na ndio inayotegemewa na jamii nzima.

"Kilichoshuka siyo ufaulu wa alama twende kwenye uhalisia wa maisha vinaendana na elimu inayotolewa kwani zamani mwanafunzi aliyemaliza kidato cha sita zamani alikuwa anakusanya watoto mtaani anawafundisha kwasasa huwezi kukuta kwasasa mwalimu hata Mkurugenzi anaiba mtihani ili tu aongeze ufaulu si sawa alama hizi zipo tu,"amesisitiza Dkt. Mkanachi.

Hata hivyo amewaagiza Maafisa Elimu Msingi na Sekondari kukaa na Wakuu wa Shule na Walimu Wakuu mmoja mmoja ili kusikiliza changamoto zao na wanachotaka ikiwa ni pamoja na kuwapa wao wanachotamani kutoka kwao ili waweze kupiga hatua kwa pamoja.

Hafla ya uzinduzi wa kitabu cha Mkakati wa kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji ngazi ya elimu msingi na kitabu cha Changamoto katika uboreshaji elimu msingi na Sekondari umefanyika baada ya kuzinduliwa kitaifa na kimkoa na umehudhuriwa na Kaimu Mkurugenzi.

# Watumishi Halmashauri ya Mji wamshukuru Mhe. Rais



**Mhe. Samia Suluhu Hassan**
**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

Watumishi katika Halmashauri ya Mji Kondoa wamemshukuru Rais Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuwaongezea mishahara na kuwapandisha madaraja hali ambayo itawaongezea hali ya ufanyaji kazi.

Shukrani hizo wamezitoa walipokuwa wakiongea na wanahabari katika ofisi za Halmashauri ya Mji Kondoa hivi karibuni.

Akiongea kwaniaba ya wakuu wa Idara, mkuu wa Idara ya Kilimo na Mifugo Hassan Kiseto amesema anamshukuru Mhe. Rais kwa uwezeshaji wa miradi mbalimbali katika sekta ya elimu, afya, kilimo na sekta zingine.

"Yapo madarasa, vituo vya afya na zahahati ambavyo vimekamilika na baadhi vmeanza kutoa huduma na hii yote ni kuzipa kipaumbele sekta hizo na zingine lengo likiwa ni kutoa huduma kwa wananchi," amesema Bw. Kiseto

Ameongeza kumshukuru Mhe. Rais kwa kuwawezesha watumishi kwa kuwaongezea mishahara asilimia 23.3 kwa kima cha chini hali ambayo imewezesha watumishi kufurahia mishahara yao ikiwa ni pamoja na watumishi wa mishahara ya kati na juu.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Chama cha Walimu Wilaya ya Kondoa Mwalimu Ntomola amesema anamshukuru kwa niaba ya walimu wa Kondoa kwa kuwapandisha madaraja kwa kuwa kwa kipindi kirefu walikuwa hawajapandishwa ikiwa ni pamoja na kulipwa mishahara inayoendana na madaraja yao.

"Mama ameonyesha upendo wa dhati kwa kuwajali walimu wa kima cha chini na kulipa malimbikizo ya mishahara na kama wamebakia ni wachache sana huo ni upendo wa dhati kwa walimu na wao pia wameonyesha kuridhika na kushukuru kwa kuwa wanasema usiposhukuru kwa kidogo huwezi kushukuru kwa kikubwa,"amesisitiza Mwalimu Ntomola

Hata hivyo amewasihi walimu kutosikiliza maneno ya pembeni kwani hayatawajenga kwa kuwa amewaheshimisha na ana imani Mhe.Rais ataongeza zaidi ya kilichotolewa na kumuomba kuendelea kuwakumbuka walimu kwa kuwa ni daraja la sekta zote.

Naye Thobias Mmary mmoja wa watumishi waliopandishwa daraja na kupata nyongeza ya mshahara amesema alichokipata ni kikubwa kwa kuwa kitamuongezea uwezo wa kupata mkopo atakaoutumia kwa shughuli zake binafsi za kujiongezea kipato ili kujiinua kiuchumi.

Mhe. Rais kwa alilolifanya amerudisha heshima ya mtumishi wa umma na niwasihi watumishi wenzangu tushukuru kwa kilichopatikana penye mapungufu serikali itapafanyia kazi kama alivyoongea Waziri Mkuu Mhe. Kassimu Majaliwa,"ameongeza Mmari

Halmashauri ya Mji Kondoa ina zaidi ya watumishi 840 ambapo zaidi ya watumishi 153 wamepandishwa madaraja.



# Wafanyabiashara Kondoa watakiwa Kutumia fursa kukua kiuchumi

Mkuu wa Wilaya ya Kondoa Dkt. Khamis Mkanachi amewataka wafanyabiashara wa Wilaya ya Kondoa kutumia fursa mbalimbali zilizopo wilayani humo kwa kuwa mazingira yameboreshwa hali ambayo itawafanya hao wakue kimtaji na kuwa wafanyabiashara wakubwa.

Kauli hiyo ameitoa wakati wa kikao na wafanyabiashara, wataalam wa Mamlaka ya Mapato Tanzania na Halmashauri wilayani humo kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Kondoa Irangi hivi karibuni.

“Bomba la mafuta linakuja tumieni fursa hiyo kwa kuungana pamoja na kufanya vitu kwa pamoja ili muweze kutoa huduma mbalimbali kwa wafanyakazi wa bomba la mafuta ikiwa ni pamoja na kununua gari la kubebea maji taka ambalo hakuna kwasasa mtapata kipato na pia wananchi watahitaji huduma yenu,”amesema Dkt. Mkanachi

Aidha amewasihi kuendelea kuwekeza katika sekta ya utalii kwa kuwa kwa sasa mazingira yameboreshwa katika hifadhi ya Mkungunero ambapo inapokea wageni wanaokuja kwa ajili ya kutalii na wanahitaji sehemu za kupumzika hivyo ni wakati wao kujenga hoteli za kisasa zitakazowavutia na wao kujipatia fedha na kukua kichumi.

Aidha amewataka Mamlaka ya Mapato Tanzania kuacha kuwasumbua wafanyabiashara ili wafanye biashara zao kwa utulivu na kutumia lugha nzuri pindi wanapoenda kukusanya kodi ikiwa ni pamoja na kuwatoza tozo wanazostahiki kulipa.

“TRA najua mna utaratibu wenu wa kutoa elimu hivyo mjipange vizuri na wakati mnakusanya mapato inategemea mnaendaje suala la kutoa fedha si rahisi linahitaji ushawishi sasa kama hauna lugha nzuri ya ushawishi nitakupa hela? Hapana siwezi kutoa fedha hebu twende vizuri tuwashirikishe ili watupe kodi tunazozihitaji,”amesisitiza Dkt. Mkanachi.

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa Ndg. Paul Sweya amewataka vijana chini ya miaka 35 kujiunga katika vikundi na kuomba mikopo kutoka Halmashauri ambayo inatolewa kila robo mwaka na kuwasisitiza kuwa kwasasa mikopo inatolewa kwa njia ya mtandao na elimu ya jinsi ya kuomba inaendelea kutolewa.

Akitoa elimu ya mlipa kodi Afisa Usimamizi Kodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania Ndg. Philipo Eliamini amesema kodi wanayopaswa kulipa inatokana na faida ya mauzo kwa mwaka na kila mfanyabiashara analipa kulingana na biashara yake na ndio maana kuna wafanyabiashara wakubwa, kati na wadogo.

“Mfanyabiashara ambaye mauzo yake ni chini ya shilingi milioni nne hawawajibiki kulipa kodi TRA anachukuliwa kama mjasiriamali mdogo, mauzo ya milioni nne hadi saba kodi yake ni milioni moja, milioni saba hadi 11 kodi milioni mbili na nusu, milioni kumi na mbili hadi milioni 99 atalipa asilimia 3.5 ya mauzo yake,”amesema Ndg.Philipo

Kwa upande wao wafanyabiashara wameushukuru uongozi kwa kikao hicho cha kuwakutanisha pamoja ambapo pia wamepata fursa ya kuelezea changamoto zao na wameomba kiwe kinafanyika mara kwa mara na wamefahamu mambo mbalimbali kuhusu ulipaji kodi na umuhimu wake hivyo wataenda kuwa mabalozi kwa wengine katika kulipa kodi.

Kikao cha Mkuu wa Wilaya na wafanyabiashara kimefanyika kwa lengo la kuwakutanisha lakini pia kuwapatia elimu ya mlipa kodi.



# Mwenge wa Uhuru Wakamilisha salama mbio zake Wilaya ya Kondoa

Mwenge wa Uhuru umemaliza mbio zake wilayani Kondoa na kupokelewa na Mkuu wa Wilaya ya Chamwino Mhe. Gift Msuya ambapokatika wilaya ya Kondoa umepitia miradi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa na Halmashauri ya Mji Kondoa.

Mwenge wa uhuru katika Halmashauri ya Mji Kondoa umepitia miradi 5 yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 2.1 iliyopo katika kata ya Kilimani, Serya, Kingale na Kondoa Mjini na miradi yote iliwekewa mawe ya msingi na kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa Ndg.Sahili Nyanzabara Geraruma.

Akiwaaga wanakondoa kabla ya kwenda Chamwino Mkimbiza Mwenge kitaifa Ndg. Sahili Geraruma amewashukuru kwa ukarimu wao na kuwataka kila mtumishi kufanya kazi kwa kufuata misingi ya taaluma yake ili kuhakikisha huduma kusudiwa inawafikia wananchi kwa viwango vya hali ya juu.

" Aidha nawasihi sana ifikapo 23 Agosti 2022 wananchi wote tutoe tushiriki katika zoezi la kitaifa la sensa ya watu na makazi kwa kuonyesha ushirikiano kwa makarani wa sensa ili malengo ya serikali yatimie,"amesema Ndg. Geraruma

Aidha mwenge umekesha katika viwanja vya Sabasaba Kata ya Chemchem ambapo shughuli mbalimbali zilofanyika ikiwemo upimaji wa VVU, uchangiaji wa damu, chanjo ya UVICO 19, elimu ya lishe na ugawaji wa kondomu za kike na kiume.



Akisoma matokeo upimaji wa VVU Mkuu wa Wilaya ya Kondoa Dkt. Khamis Mkanachi amesema jumla ya watu 385 walipima na watu 2 wamekutwa na maambukizi ambapo ni sawa na asilimia 0.5, watu 53 wamechangia damu, watu 137 wamepata chanjo ya UVICO 19, watu 565 wamepata elimu ya lishe na kondomu 16400 zilichukuliwa na watu.



# “Simamieni sheria Ukusanyaji wa mapato”Mkurugenzi

Watendaji wa kata na mitaa Halmashauri ya Mji Kondoa wametakiwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu wakati wa kukusanya mapato ili kuepuka migogoro isiyokuwa na tija na wafanyabiashara.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi wa Halmashauri Paul Mamba wakati wa kikao cha kuweka mikakati ya kukusanya mapato kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa halmashauri hivi karibuni.

"Nawasihi sana tukasimamie sheria na kuacha uzembe katika kukusanya mapato lakini pia msimwonee mtu wakati wa ukusanyaji wa mapato na watendaji wa kata mtendaji wa kata asiyewajibika mwambie ili ajirekebishe,"amesema Mkurugenzi Mamba

Aidha amemwagiza Mweka Hazina kuhakikisha anawapatia motisha watendaji hao wanapowasilisha mapato kwa mwezi ili kuwasaidia wakati wa ukusanyaji wa mapato na kuwafuatilia wote wanaochelewesha mapato.

"Tubadilike na tufanye kazi na kuyafanyia kazi yale tunayoagizana na ndio maana nimewaita leo mseme changamoto zinazowakabili ili turekebishe mapema na tunawekeana malengo ya ukusanyaji ili tufikie malengo tuliyojiwekea katika bajeti,"amesisitiza Mkurugenzi Mamba

Akiongea kwa niaba ya watendaji wengine Samson Mtui Mtendaji wa Kata ya Kondoa Mjini amesema wanaenda kusimamia yote waliyokubaliana na kuanza upya ili kufikia malengo ya Halmashauri.

Kikao cha watendaji kimefanyika ili kuimarisha na kupeana mbinu za ukusanyaji wa mapato ambapo Mkurugenzi amewasihi pia kuendelea kuiongelea agenda ya lishe katika mikutano ya maeneo yao ya utawala na kimehudhuriwa pia na Mkuu wa Idara ya Utumishi na Kaimu Mkuu wa kitengo cha Fedha.



# "Wakulima jiandikisheni daftari la ruzuku ya mbolea"- Afisa Kilimo

Wakulima Halmashauri wametakiwa kujiandikisha kwenye daftari la ruzuku ya mbolea yanayopatikana kuanzia leo kwa maafisa ugani katika mitaa ili kupata mbolea ya ruzuku msimu wa kilimo utakapoanza.

Hayo yamesemwa na Mkuu wa Idara ya Kilimo na Mifugo Ndg. Hassan Kiseto alipokuwa akitoa ufafanuzi wa upatikanaji wa mbolea ya ruzuku wakati wa kikao cha wafanyabiashara na Mkuu wa Wilaya kilichofanyika katika Ukumbi wa Kondoa Irangi hivi karibuni.

"Daftari hili litatumika kuwasajili wakulima wote wanaofanya shughuli za kilimo ndani ya eneo la Halmashauri ya Mji Kondoa ili wapate namba zitakazowawezesha kwenda kwenye maduka ya mawakala waliochaguliwa kutoa mbolea za ruzuku na wao wakulima watalipa fedha kiasi na serikali itatoa kiasi na namba hizo zitakuwa kwenye mfumo,"amesema Ndg. Kiseto

Aidha amesema kutokana na vita inayoendelea ya Ukraine gharama za mbolea zimepanda hivyo serikali itampunguzia mzigo mkulima atakayejisajili katika daftari kwa kumlipia kiasi cha fedha na yeye mwenyewe atalipa fedha nyingine lengo ni kuhakikisha wakulima wanaendelea na shughuli zao za uzalishaji kwa gharama nafuu.

Madaftari hayo yanapatikana kwa Maafisa Ugani wa mitaa wote na kwa mitaa isiyo na mafisa ugani wametakiwa kuwasilisiliana na maafisa Ugani wa kata ili wawaelekeza madaftari yanapopatikana aidha uandikishaji huo ni bure kwa wakulima wote.



# Aliyevamia eneo la stendi Bicha apewa siku saba kuvunja nyumba

Mwananchi aliyejulikana kwa jina la Mohamed Fonga aliyevamia na kujenga eneo la mradi wa viwanja vya stendi ya Bicha amepewa siku saba kuvunja nyumba aliyojenga kwa kuwa alishapewa fidia ya eneo hilo shilingi milioni 40 hapo awali.

Kauli hiyo imetolewa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa Ndg. Paul Mamba Sweya wakati kamati ya fedha na Utawala kwa ajili ya kukagua mali za Halmashauri ilipofika kukagua eneo la mradi wa stendi ya Bicha hivi karibuni.

"Cha pili tunamtaka arudishe mabati aliyoiba katika choo cha stendi, matofali na fremu tatu za milango zilizokuwepo katika eneo la mradi na sitaki kumuona ofisini kwangu kuhusu suala la hapa ila akija kama mwananchi mwingine nitamuhudumia kwanza tumefahamiana kwa kuwa migogoro wakati mwingine inaleta hali ya kufahamiana,"amesema Mkurugenzi Sweya

Aidha amemtaka kutekeleza agizo la kuijibu barua aliyomwandikia Mhe. Mkuu wa Mkoa na Mhe. Mkuu Wilaya akimshukuru kumrudishia eneo lake na nakala ampatie Mkurugenzi ikiwa ni pamoja na kuwaomba msamaha viongozi kwa kuwa aliwadanganya.

"Tukiruhusu viongozi wetu ambao Mhe. Rais anawateua watumike vibaya sababu ya ujuaji hatuwezi kufika mbali na kwa vile nimeona umuhimu wa hili tuna viongozi wa TAKUKURU hapa na OCD ametuma watu wawili hili suala lisipo tekelezwa Mwanasheria mchukue hatua wizi wa mabati,matofali, uvunjaji wa becon na miti tuliyoilipia ikachukuliwa virejeshwe hapa,"amesisitiza Mkurugenzi Sweya

Akiongea Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Mhe. Mohamed Kiberenge amesema maagizo ya Mkurugenzi yatekelezwa sababu ni agizo la kiutendaji na kuwataka waliokuwa wakilalamika wkatekeleze maagizo na mambo mengine ambayo yapo kisheria yakaendelee.

"Naomba sasa hili lifike mwisho na mradi uendelee kama tulivyokubaliana na hii ni kamati ya fedha ambayo inasimamia mali za Halmashauri kwa kushirikiana wataalam na madiwani kwa hiyo niwaombe sasa nyie mna nafasi ya kuzungumza na wanasheria kwa sababu sisi ni vyombo vinasimama na nyie hatuna muda wa kusikiliza kesi tena kwasababu tulisha maliza na kuwalipa fidia kwa hiyo mtaendelea kukiri kwenye vyombo,"amesisitiza Mhe. Kiberenge.



# "Taarifa utazotoa kwa karani ni siri" - Dkt. Mkanachi

Mkuu wa Wilaya ya Kondoa Dkt. Khamisi Mkanachi amewahakikishia wananchi wa Kondoa kuwa taarifa watakazotoa ni siri kati yao na makarani wa sensa na zitatumika kwa ajili ya kupata takwimu zitakazopelekea serikali kupanga mipango yake na si vinginevyo.

Kauli hiyo ameitoa wakati wa tamasha la kuhamasisha sensa ya watu na makazi lililofanyika katika uwanja Sabasaba Kondoa Mjini.

"Mkae mkifahamu kuwa taarifa hizi hazitumiki kwa namna yoyote zaidi ya kitakwimu tu kupanga mipango ya kiserikali sawasawa usije ukahofisha sasa ukaanza kudanganya ukajiwekea mambo makubwamakubwa kumbe hayapo au ukafichaficha kumbe vipo utatukwaza kama serikali maana tutashindwa kupanga mipango yetu ya maendeleo kwa watu wetu,"amesema Dkt. Mkanachi

Aidha amewataka washiriki wa bonanza hilo kwenda kutoa ujumbe sahihi juu ya sensa kwa kuelezea maswali yatakayoulizwa siku ya sensa na kuongeza kuwa watakaopita kuchukua taarifa ni makarani wa sensa waliopewa mafunzo ambapo zaidi ya wataalam laki mbili wamepewa mafunzo na kwa Wilaya ya Kondoa ni wataalam zaidi ya elfu moja watashiriki kwa fedha za serikali hivyo jambo hilo ni muhimu kwa kuwa serikali imetenga fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji.

"Makarani watakaokuja watakuwa wamevaa sare maalum hawatavaa kama mimi hapa track suit na watakuwa na vitambulisho hatakuja mtu kutoka sehemu yoyote na hatakuwa peke yake atakuwa na Mwenyekiti wako wa mtaa au kijiji na watakuwa wamechukua tahadhali zote ya kujikinga na UVIKO 19 kwa hiyo hakuna atakayeambukizwa na atakayemwambukiza karani wetu. zoezi litakwenda vizuri na litakamilika,"amesisitiza Dkt. Mkanachi

Naye mbunge wa Kondoa Mjini Mhe. Ally Makoa amesema wananchi wengi wanaelimu ya sensa jambo lililobakia ni kuendelea kutoa elimu kwenye vikao na mikutano ili waendelee kupata elimu na kuongeza kuwa upatikaji wa takwimu hizo utasaidia kupata miradi ya maendeleo ikiwemo mradi wa uendelezaji wa miji TACTIC ambao idadi ya watu ni kigezo muhimu kwa ajili ya kupata miradi hiyo.

Bonanza hilo limefanyika ikiwa ni mwendelezo wa zoezi la kutoa elimu ya sensa ambapo Mkuu wa Wilaya aligawa vipeperushi kwa makundi mbalimbali na kushiriki katika zoezi la ukimbiaji katika maeneo ya mjini na mpira wa mguu kati ya timu ya Wasafi na Sensa Spesho ambapo timu zote zilifungana goli 2 na lilihudhuriwa na watumishi wa taasisi za serikali na wananchi wa wilaya ya Kondoa.

# MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2021/2022



Madarasa mawili Shule ya Msingi Mongoroma kwa gharama ya shilingi milioni 40 Fedha kutoka Serikali kuu.



Mradi wa maji na sehemu ya kunawia mikono wanafunzi shule ya Msingi Mongoroma kwa gharama ya shilingi milioni 11.8 Fedha kutoka Serikali kuu UVIKO 19



Darasa moja Shule ya Msingi Mongoroma kwa gharama ya shilingi milioni 20 Fedha kutoka Serikali kuu.



Umaliziaji wa maabara mbili Shule ya Sekondari Kolo kwa gharama ya shilingi milioni 60 fedha kutoka Serikali kuu.



Umaliziaji wa maabara Shule ya Sekondari Mtobubu kwa gharama ya shilingi milioni 60 fedha kutoka Serikali kuu



Ujenzi wa madarasa mawili Shule ya Msingi Mulua kwa gharama ya shilingi milioni 40 fedha kutoka Serikali kuu.

# MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2021/2022



Jengo la maabara kituo cha Afya Serya moja ya jengo katika kituo cha Afya Serya ambapo imetolewa shilingi milioni 500.



Jengo la Zahanati Mongoroma kabla ya kujengwa Kituo cha Afya Serya



Ujenzi wa Zahanati ya Chandimo kwa gharama ya shilingi milioni 50 fedha kutoka mapato ya ndani ujenzi unaendelea



Ujenzi wa Zahanati ya Mulua kwa gharama ya shilingi milioni 50 fedha kutoka Serikali kuu ujenzi unaendelea



Ujenzi wa Zahanati ya Ausia kwa gharama ya shilingi milioni 50 fedha kutoka mapato ya ndani ujenzi unaendelea.



Ujenzi wa Zahanati ya Hachwi kwa gharama ya shilingi milioni 50 fedha kutoka Serikali kuu ujenzi upo hatua ya ukamilishaji.

# MATUKIO MBALIMBALI KATIKA KIKAO CHA BARAZA LA WAHESHIMIWA MADIWANI ROBO YA NNE 2021/2022



Mhe. Japhari Ganga (kushoto) akiwa na Mhe. Issa Kambi wakiangalia taarifa kwenye kishikwambi ikiwa ni mara ya kwanza kutumia



Mhe. Zainabu Haroub (kushoto) akiwa na Mhe. Ramla Abeid wakiangalia taarifa kwenye kishikwambi ikiwa ni mara ya kwanza kutumia



Mhe. Mohamed Kiberenge (katikati) akiendesha kikao cha baraza la Waheshimiwa madiwani



Maheshimiwa wakiperuzi taarifa kutoka kwenye vishkwambi katika baraza la waheshimiwa madi-wani robo ya nne




Makamu Mwenyekiti Mhe. Besela Maunga akichangia mada wakati wa kikao cha baraza la Waheshimiwa madiwani



Mhe. Fatuma Issa akichangia hoja katika kikao cha Baraza la Waheshimiwa madiwani robo ya nne

# MATUKIO MBALIMBALI YALIYOFANYIKA KATIKA ROBO YA KWANZA MWAKA WA FEDHA 2022/2023



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Kondoa Mhe. Mohamed Kiberenge akisisitiza jambo wakati wa ziara ya Waheshimiwa Madiwani wa kamati ya Fedha kukagua mali za Halmashauri



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa Ndg. Mustapha Semwaiko (kushoto) akimkabidhi Mwenge wa Uhuru Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa Ndg. Paul Sweya



Waheshimiwa Madiwani wa kamati ya Fedha na wataalam wakikagua mipaka ya Chuo Cha Ualimu Bustani wakati wa ziara ya Waheshimiwa Madiwani kukagua mali za Halmashauri



Kiongozi wa mbio za Mwenge kitaifa Ndg.Sahili N. Geraruma akiweka jiwe la Msingi katika kituo cha Afya Serya wakati wa mbio za Mwenge Kondoa



Waheshimiwa Madiwani wa kamati ya Fedha wakiangalia kilichokuwa choo kwenye eneo la wazi kwa ajili ya soko mtaa wa Iboni



Viongozi na Watumishi mbalimbali wa Halmashauri ya Mji Kondoa wakicheza na kuimba katika eneo la mapokezi ya Mwenge Bicha Mnadani